



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MADINI

**USHIRIKISHWAJI WA WATANZANIA
KATIKA RASILIMALI MADINI NA
UWAJIBIKAJI WA MAKAMPUNI
KWA JAMII(LC&CSR)**



USHIRIKI WA WATANZANIA (LC)

Jumla ya Thamani inayoongezwa au kutengenezwa katika uchumi wa nchi yetu kutokana na uamuzi wa makusudi wa kutumia watanzania (Ajira) pamoja na bidhaa na Huduma za hapa nchini katika mnyororo mzima wa thamani katika Sekta ya Madini (utafiti, uchimbaji, uchenjuaji na biashara ya madini)

Ushiriki wa Watanzania umeibua na kuchochea fursa mbalimbali katika nafasi za ajira na mafunzo, uhawilishwaji wa teknolojia, utafiti na maendeleo, matumizi ya huduma na bidhaa zinazozalishwa nchini na zile zinazotolewa na Watanzania.

Kwa mujibu wa Sheria ya Madini, 2010 na Marekebisho yake yaliyofanyika Mwaka 2017; Vifungu vya 102 – 104 vya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 Sura 123 vinaelezea kuhusu LC.

Kifungu cha 102 (1) cha sheria ya Madini

Kinamtaka Mmiliki wa leseni kutoa kipaumbele cha kutumia bidhaa zinazozalishwa au zinazopatikana ndani ya Tanzania pamoja na huduma zinazotolewa na watanzania au kampuni za kitanzania.

Kifungu cha 102 (2) na (3) cha sheria ya Madini

Kinaeleza kuwa; endapo bidhaa zinazohitajika na mmiliki wa leseni Tanzania, bidhaa hizo zitolewe na kampuni ya ndani kwa kuingia ubia na kampuni ya kigeni. Kampuni hiyo ya ndani itamiliki hisa zisizopungua, asilimia ishirini na tano (25%) katika ubia huo.

Wajibu wa mmiliki wa leseni kwa jamii (CSR)

CSR ni: Wajibu wa mmiliki wa leseni kwa jamii inayomzunguka mgodi. CSR ni mkakati ambao **Mmiliki wa Haki ya Madini (PML, PL, ML, SML & PCL)** anaweka kwenye mpango kama sehemu ya utawala wa ushirika (corporate governance) ambao umeandaliwa ili kuhakikisha mmiliki wa leseni anafanya kazi kwa maadili na kwa manufaa ya jamii husika;

Kifungu cha 105 (1) na (2) cha Sheria ya Madini

Kinamtaka mmiliki wa leseni, kuandaa mpango wa mwaka wa Wajibu wake kwa Jamii uliofikiwa kwa pamoja na Halmashauri husika kwa kushauriana na Waziri anayehusika na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Waziri wa Fedha.

Aidha, Mpango huo unaoandaliwa uzingatie masuala ya mazingira, kijamii, kiuchumi na kitamaduni kulingana na vipaumbele vya Halmashauri ya jamii inayozunguka mgodi.

Kifungu cha 105 (3) cha Sheria ya Madini.

Mmiliki wa leseni anapaswa kuwasilisha kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa husika Mpango wa Wajibu wake kwa Jamii alioandaa kwa ajili ya kufanyiwa tathmini na kupata idhini.

Kifungu cha 105 (4) cha sheria ya Madini

Kinaeleza kuwa, kila Halmashauri zinatakiwa kufanya yafuatayo:
Kuandaa miongozo (guidelines) ya Wajibu wa Mmiliki wa Leseni kwa Jamii kwenye Miradi ya maendeleo katika maeneo yao;
Kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Wajibu wa Mmiliki wa Leseni kwa Jamii (CSR Plan).

Kutoa elimu kwa jamii kuhusu miradi ya maendeleo katika maeneo yao.

Kifungu cha 105 (5) cha sheria ya Madini

Kinatafsiri jamii husika ya eneo linalozunguka mgodi kuwa ni wakazi wa maeneo ambapo shughuli za uzalishaji madini zinafanyika.



Wasiliana nasi kupitia anwani ifuatayo:

**Wizara ya Madini,
Mji wa Serekali– Mtumba,
S.L.P 422,
DODOMA.**

**Simu: +255 26230051,
Nukushi: +255 26 2322282
Barua Pepe: ps@madini.go.tz
Tovuti: www.madini.go.tz**

